AKA 1972>>Yalijengwa machinjio ya nyama eneo la Kariakoo, Tabora

# RC Tabora atoa siku mbili machinjio yafanyiwe usafi

**Na ALLAN KITWE,** *Tabora*

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Batilda Burian, amempa siku mbili Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Bosco Ndunguru, kuhakikisha machinjio ya nyama yaliyoko eneo la Kariakoo, yanafanyiwa usafi.

Agizo hilo alilitoa mwishoni mwa wiki alipotembelea na kukagua mazingira ya machinjio hayo na kubainisha kuwa hali ya usafi katika machinjio hayo hairidhishi.

"Sakafu, kuta na mifereji ya kutolea uchafu ni vichafu, vyombo vya kuhifadhia nyama navyo haviridhishi ikiwemo uchakavu wa miundombinu," alieleza.

Alisema lengo la kujengwa machinjio hayo ni kuongeza vyanzo vya mapato, lakini kwa hali ilivyo sasa malengo hayo hayawezi kufikiwa na kuagiza maboresho yafanyike ikiwemo kuanzisha vyanzo vingine vya mapato.

Batilda alimtaka mkurugenzi huyo kutoridhika na mapato wanayopata bali wafanye kila linalowezekana kuhakikisha lengo la machinjio hayo kuwa kitovu cha kusafirisha nyama katika mataifa jirani ya Burundi na Rwanda linatimizwa.

"Fanyeni usafi wa kina, nawapa siku mbili mandhari ya machinjio haya yabadilike, pakeni rangi kuta zote, wekeni marumaru na maboksi yote ya kuwekea nyama yawe safi, sitaki mniangushe," alisema.

Aliwataka kutumia sehemu ya mapato wanayokusanya kuboresha eneo hilo wakati wakisubiri mradi wa Benki ya Dunia ambao utahusisha pia ujenzi wa machinjio hayo kuwa ya kiwango cha kisasa.

Mkuu wa Wilaya ya Tabora Mjini, Dk. Yahaya Nawanda, alimhakikishia Mkuu wa Mkoa huyo kwamba atafanyia kazi maelekezo yote aliyoyatoa haraka iwezekanavyo kuhakikisha machinjio hayo yanakuwa na mwonekano mzuri ili kuongeza mapato.

Awali, akitoa taarifa kuhusu machinjio hayo, Mkurugenzi Ndunguru alisema machinjio hayo yaliyojengwa kwa ufadhili wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Ulaya mwaka 1972, yanakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa miundombinu.

## Mkoa wa Simiyu ipanga kuongeza zalishaji pamba

**TANTINE MATHIAS,** *Simiyu*

l Mkoa wa Simiyu, imesema imeandaa wa kuongeza uzalishaji wa zao la pamba go la kufikia tani laki tano msimu ujao wa 2022/2023.

kana na mkakati huo, Mkuu wa Mkoa avid Kafulila, amewaagiza wakuu wa a wakurugenzi kubainisha mikokoteni jiji na vitongoji ili iwasaidie kusambaza za samadi shambani kwa maandalizi ya simu ujao.

lila aliyasema hayo mwishoni mwa wiki inisha kwamba mkakati wa mkoa huo simu ujao ni kuzalisha tani laki tano lenga usambazaji wa mbolea ya samadi haukwepeki na upandaji wa kitaalamu mia kamba.

halmashauri landae bajeti ya usambazaji lea ya samadi, haya maandalizi yote va tuyafanye kipindi hiki kwa kuainisha ambayo samadi inapatikana na

> ka kuona kila mdau ba anahusika katika dia mkulima katika zaji wa mbolea, kutoa kilimo, upandaji, i, upuliziaji hadi uvunaji
>
> Mkoa David Kafulila

ambayo yatapatiwa samadi,"

a viongozi hao kuhakikisha mpango ilika kabla ya Julai mosi, mwaka akiwasihi wanunuzi wa pamba na serikali, wakulima na maofisa kikisha wanamsaidia mkulima bazaji wa samadi hadi uvunaji.

kuona kila mdau wa pamba atika kumsaidia mkulima katika a mbolea, kutoa elimu ya kilimo, palliliaji, upuliziaji hadi uvunaji,"

lisema lengo la wadau wote wa rikiana ni kuhakikisha malengo ya i laki tano yanafikiwa, badala ya kulima wazalishe bila tija.

a Mkoa huyo pia aliitaka Bodi ya kikisha wanatimiza wajibu wao kwa ora wa pamba kutoka kwa wakulima, shirika na viwandani.

MIFUGO



MKUU wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Buriani (wa tatu kushoto), akipata maelezo kutoka kwa muuzaji wa ng'ombe wa mbegu kutoka Biharamulo, Haruna Mazoea (kushoto), wakati wa ziara ya kukagua ukusanyaji wa mapato na kutoa tahadhari dhidi ya virusi vya corona, katika Mnada wa Ipuli, mwishoni mwa wiki.(Picha na Tiganya Vincent).

## Shigella aingilia kati mgogoro wa wananchi na mwekezaji

**Na IGAMBA LIBONGE,** *Kilombero*

kilimo wanapokwenda kulima eneo hilo, mwekezaji anatumia askari polisi

Mkoa wa Morogoro Loata Ole Sanare, alitoa maelekezo kwa mwekezaji

Scanned with CamScanner




# Mwanga mpya wamulika kwenye mifugo, uvuvi

Na Selemani Nzaro

KATIKA siku 100 Serikali ya Awamu ya Sita imefanya mambo makubwa kwenye sekta za mifugo na uvuvi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel anasema kazi hizo zimetokana na maelekezo ya Rais Samia aliyoyatoa katika hotuba zake kwenye matukio tofauti akilenga kuboresha sekta za mifugo na uvuvi.

Profesa Ole Gabriel anasema baada ya kuingia madarakani, Rais Samia alionesha kusikitishwa na hali ya mifugo ilivyo nchini kutokana na kutonenepa pamoja na wafugaji wake.

Anasema changamoto hiyo inatokana na mifugo na wafugaji kutembea umbali mrefu kutafuta malisho pamoja na maji na wakati mwingine wasifanikiwe, hali inayosababisha mifugo yao kudhoofika.

Anasema serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeamua kuikabili changamoto hiyo kwa kutenga, kupima na kuweka katika gazeti la serikali maeneo ya malisho.

Hadi sasa kuna jumla ya hekta milioni tatu za malisho na lengo ni kufikia hekta milioni sita ifikapo mwaka 2025.

Profesa Ole Gabriel anasema serikali inatoa elimu kwa wafugaji namna ya kuwa na akiba ya malisho kwa kulima na kuhifadhi malisho ili wawe na uhakika wa malisho kwa mifugo yao mwaka mzima.

Anasema wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa malisho, kutoa mafunzo rejea kwa wakaguzi 79 wa maeneo ya malisho; na kuimarisha mashamba ya Serikali ya kuzalisha malisho na mbegu kwa kuyapatia vitendea kazi ili kuongeza uzalishaji wa mbegu.

Profesa Ole Gabriel anasema wizara imewasiliana na ofisi ya ubalozi wa Tanzania nchini China na wadau wa sekta binafsi kwa ajili ya mkakati maalumu wa kuzalisha mbegu za majani ya Juncau kutoka China. Mpango huu utakuwa mkombozi kwa wafugaji.

Kwa upande wa kutatua changamoto ya ukosefu wa maji kwa ajili ya mifugo, Profesa Ole Gabriel anasema katika siku 100 ya Rais Samia, wizara imejenga visima virefu viwili huko Usolanga na Mpapa katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa na vimefikia asilimia 70 na 30.

Anasema wizara imekarabati mabwawa matatu ya Chamakweza huko Chalinze, Kimokoua wilayani Longido na Narakauo wilayani Simanjiro ambayo yote yamekamilika kwa asilimia 100.

Serikali imetoa mafunzo na leseni kwa wachunaji ngozi 340 wa machinjio za Manispaa ya Kinondoni na Temeke Dar es Salaam. Pia, imewapatia vitendea kazi wakaguzi wa ngozi 34 wa wilaya za Mikoa ya Mwanza, Simiyu, Shinyanga na Mara. Lengo ni kuwezesha upatikanaji wa ngozi bora kwa ajili ya viwanda.

Profesa Ole Gabriel anasema katika kipindi cha siku 100 zilizopita serikali imewezesha minada kufunguliwa.

Anasema mnada wa mifugo wa mpakani wa Magena, Mara umefunguliwa ili kuwezesha biashara ya mifugo kati ya Tanzania na Kenya. Pia, ujenzi wa mnada wa mifugo wa Buzirayombo mkoani Geita umefikia asilimia 50, lengo likiwa ni kuboresha biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi.

Kwa upande wa ushirikiano, Wizara ya Mifugo na Uvuvi hususani sekta ya mifugo kwa upande wa Serikali ya Muungano na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zimefanya kikao na kukubaliana kuendeleza ushirikiano kiutendaji katika ngazi za idara na taasisi zilizo chini ya Wizara hizo. Lengo ni kuimarisha sekta za mifugo katika pande mbili za muungano.

Kwa upande wa sekta ya uvuvi, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika siku 100 za uongozi wa awamu ya sita ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa Majengo Matatu ya Ofisi za Vikundi vya usimamizi wa Rasilimali ya Uvuvi (BMU) katika Wilaya za Pangani (Kipumbwi), Mkinga (Zingibari) na Bagamoyo (Dunda).

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia uvuvi, Dk Rashid Tamatama anasema Serikali ya Awamu ya Sita katika siku 100 imeboresha miundombinu wezeshaji ya shughuli za uvuvi kwa kuanza ujenzi wa mialo sita katika Kanda ya Ziwa, ujenzi wa soko la samaki la Mbamba Bay mkoani Ruvuma, na kutangazwa kwa zabuni ya kupata Mkandarasi wa Ukarabati wa Soko la Samaki la Feri mkoani Dar es Salaam utakaoanza Julai 2021.

"Katika kipindi hicho tumeshuhudia kutengwa kwa fedha za ndani shilingi bilioni 50 katika bajeti ya 2021/2022 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo la Mbegani wilayani Bagamoyo pamoja na kuzinduliwa kwa Dawati la Jinsia katika Sekta ya Uvuvi ili kuwawezesha wanawake kushiriki ipasavyo katika uchumi wa buluu kupitia Sekta ya Uvuvi," anasema Dk Tamatama.

Anasema mafanikio mengine katika siku 100 ambazo Rais Samia amekaa madarakani ni pamoja na kuundwa kwa kanuni mpya za kusimamia na kuendeleza uvuvi wa bahari kuu ambazo zimetayarishwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 334 la tarehe 23 Aprili, 2021.

Vilevile Serikali ya Awamu ya Sita pia imafanikiwa kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo kwenye kekta ya uvuvi kupitia mikutano ya kitaifa iliyojumuisha wageni kutoka Ufalme wa Saudi Arabia, Jamhuri wa Watu wa China, na Umoja wa Falme za Kiarabu.

Anasema kwa mara ya kwanza Juni 22, 2021 Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) ilikusanya Dola za Marekani 800,000, sawa na shilingi bilioni 1.84 yakiwa ni malipo ya leseni za uvuvi wa bahari kuu kwa meli 22 baada ya meli za kigeni kusitisha kuchukua leseni za Tanzania mwaka 2017/2018 kulikosababisha serikali kukosa mapato na DSFA kushindwa kujiendesha yenyewe.

# Samia na vyanzo vipya vya uchumi

Na Evance Ng'ingo

TANGU aingine madarakani, Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akihimiza ujenzi wa mifumo ya kukuza uchumi wa wananchi na taifa kwa ujumla.

Miongoni mwa mambo aliyoanza kuyafanya au kupanga ni kuingia makubaliano na Kenya katika biashara ya gesi, kuanza tena mchakato wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo na kuendelea na mchakato wa uchimbaji wa madini ya chuma na makaa ya mawe katika mradi wa Liganga na Mchuchuma.

**Bomba la Gesi kwenda Kenya**

Makubaliano ya mradi wa ujenzi wa bomba hilo la gesi kutoka jiji la Dar es Salaam mpaka Mombasa Kenya utasaidia kuboresha upatikanaji wa nishati na kushusha gharama ya gesi nchini Kenya, kuboresha uzalishaji viwandani.

Kwa kuifikisha gesi Kenya ni wazi kuwa Tanzania itauza gesi hiyo na kuingizia serikali mapato.

Gesi hiyo kutoka katika mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara imeshafikishwa katika jiji la Dar es Salaam na kuunganishwa kwenye viwanda kadhaa na nyingine inatumika kuzalisha umeme.

Mchumi Mbobezi nchini, Profesa Joseph Semboja anasema Rais Samia ndani ya siku zake 100 ameonesha umakini katika kuibua na kuendeleza vyanzo vya uchumi.

Profesa Semboja anasema hatua hiyo inaonesha miaka ijayo Tanzania itajiimarisha zaidi kiuchumi, kitu ambacho ni muhimu kwa maendeleo ya nchi.

"Rais Samia pia amerejesha na kuimarisha diplomasia ya uchumi na Kenya ambapo Tanzania na Kenya zimekubaliana kuwa na Tume ya Pamoja ya mawaziri wa nchi hizo mbili iwe inakutana mara kwa mara ili kutatua changamoto za kibiashara na uhusiano zinatazotokea.

Rais Samia alionesha nia ya dhati katika kuhakikisha vikwazo vya kiuchumi kati ya Tanzania na Kenya vinaondoshwa, hasa mzozo wa mara kwa mara katika mipaka ya nchi hizo mbili."

Kenya ni nchi ya tano kwa kuwekeza nchini Tanzania na ya kwanza kutoka ukanda wa Afrika Mashariki. Makampuni zaidi ya 400 ya Kenya yamewekeza dola bilioni 1.7 huku kampuni za Kitanzania zikiwekeza Sh biliomi 19 za Kenya.

Lengo kuu la Rais Samia ni kuhakikisha kuwa kuongeza wigo zaidi wa wastani wa biashara wa baina ya nchi hizi mbili ambao kwa sasa ni dola milioni 450 kwa mwaka.

**Bandari ya Bagamoyo**

Juni 26 mwaka huu Wakati akizungumza katika mkutano wa 12 wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) Rais Samia alisema tayari kuna mazungumzo yanayoendelea kati ya Taasisi iliyoonesha nia ya kujenga Bandari hiyo na serikali.

Rais anasema chini ya majadiliano hayo serikali itakuwa na jukumu lake hivyo hivyo kwa mwekezaji.

Ni wazi kuwa mradi huo ukikamilika utakuwa na manufaa makubwa kwa Tanzania hasa kutokana na nchi hii kuzungukwa na nchi ambazo hazina bandari kama Rwanda, Burundi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Watu wa Congo na Malawi ambao asilimia kubwa wanatumia bandari ya Dar es Salaam.

Mfanyabiashara ya usafirishaji wa mizigo kutoka Tanzania kuelekea Zambia, Samuel Vuza anasema kutokana na ukubwa wa uwekezwaji utakaofanyika katika Bandari ya Bagamoyo ni wazi kuwa Tanzania itavuna fedha nyingi kupitia bandari, lakini ifahamike kuwa mradi huo utahusisha pia ujenzi wa viwanda na hivyo kuchagiza zaidi kukua kwa uchumi wa nchi pamoja na kutoa ajira huku pia ukianzisha mji wa kisasa ndani yake.



**Mradi wa chuma na Makaa ya Mawe**

Kuhusiana na mradi wa Mchuchuma na Liganga uliopo wilayani Ludewa Mkoa wa Njombe, uamuzi wa Rais Samia wa kuendeleza mradi huo utalenga kuboresha zaidi mapato ya nchi.

Kauli ya Rais Samia kuwa kwa sasa chuma kimepanda bei katika soko la dunia ni wazi kuwa uamuzi wake wa kuhakikisha anauendeleza mradi huo, kuna fedha nyingi ambazo nchi itapata.

Upembuzi yakinifu ulishafanyika na kukamilika mwaka 2012 na kubainisha kuwa kuna tani milioni 126 za chuma na tani milioni 428 za makaa ya mawe.

Baadaye ilikuja kugundulika uwepo wa madini ya maana sana duniani, madini ya titanium na vanadium hivyo ni wazi kuwa hatua ya dhati ya Rais Samia ya kuuendeleza mradi huo, nchi itapata mapato zaidi.

Scanned with CamScanner



Jengo linalobishaniwa kati ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mwanza na Halmashauri ya Jiji la Mwanza lililoko barabara ya Kenyatta. (Na Mpiga Picha Wetu)

# Balozi Batilda achachamalia machinjio

**Na Benny Kingson, Tabora**

**MKURUGENZI** Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Bosco Ndunguru amepewa siku mbili kuhakikisha machinjio ya Kariakoo yanafanyiwa usafi.

Mkuu wa Mkoa Dk Batilda Buriani alitoa agizo hilo jana alipokagua mazingira ya machinjio hayo, akifuatana na viongozi wengine wa wilaya na halmashauri hiyo.

Dk Batilda alisikitishwa na hali aliyoikuta licha ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Suleimani Jafo kutoa maagizo ya kufanya marekebisho, lakini hakuna kilichofanyika.

Alisema hali ya usafi katika machinjio hayo hairidhishi, sakafu, kuta na mifereji ya kutolea taka ni vichafu na vyombo vya kuhifadhia nyama haviridhishi pampja na uchakavu wa miundombinu.

Alisema lengo la kujengwa machinjio hayo, ni kuongeza vyanzo vya mapato, lakini kwa hali ilivyo sasa, malengo hayo hayawezi kufikiwa hivyo akaagiza maboresho makubwa yafanyike ikiwamo kuanzisha vyanzo vingine vya mapato.

Mkuu wa Mkoa, alimtaka Mkurugenzi kutoridhika na mapato ya sasa, bali afanye kila linalowezekana kuhakikisha lengo la machinjio hayo kuwa kitovu cha kusafirisha nyama katika mataifa jirani ya Burundi na Rwanda, linatimia.

"Fanyeni usafi wa kina, nawapa siku mbili tu mandhari ya machinjio haya yabadilike, pakeni rangi kuta zote, wekeni marumaru na makasha yote ya kuhifadhia nyama yawe safi, sitaki kuikuta hali hii tena," alionya.

Aliwataka kutumia sehemu ya mapato kuboresha eneo hilo wakati wakisubiri mradi mkubwa wa Benki ya Dunia, ambao utahusisha pia ujenzi wa machinjio hayo kwa kiwango cha kisasa.

Mkuu wa Wilaya ya Tabora Mjini, Dk Yahya Nawanda alimhakikishia kuwa atafanyia kazi maelekezo aliyotoa haraka iwezekanavyo, ili machinjio hayo yapate mwonekano mzuri na kuongeza mapato.

Awali katika taarifa yake, Mkurugenzi Ndunguru alisema machinjio hayo yaliyojengwa kwa ufadhili wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Ulaya mwaka 1972 yanakabiliwa na changamoto kubwa ya uchakavu wa miundombinu hali inayosababisha usafi kutoridhisha.

FURSA ZA AJIRA

# Machinjio ya Vingunguti yalivyowatoa watu kimaisha - 4

RIPOTI MAALUMU

Mariam Mbwana, Mwananchi
mmbwana@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Uwepo wa Machinjio ya Vingunguti si tu unasaidia watu kupata kitoweo na mahitaji mengine, la hasha, eneo hili pia linafanya watu wengi kujipatia riziki zinazowawezesha kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo na kimaisha kwa ujumla.

Jasmini Abdi (41), mjane alianza kujishughulisha na usindikaji wa damu zinazotoka machinjioni tangu mwaka 2000 akiwa binti mdogo aliyetoka kijijini kuja kufanya kazi za ndani.

Anaeleza kuwa biashara hiyo aliirithi kutoka kwa mama aliyekuwa bosi wake ambaye alikuwa akijishughulisha na uchakataji wa damu kwa ajili ya kutengeneza kirutubisho hicho muhimu katika chakula cha kuku.

"Nilianza biashara hii nikiwa binti mdogo, nilikuwa hata sijaolewa. Niliianza kwa kumsaidia bosi wangu nilipokuwa nikifanya kazi, baadaye na mimi binafsi nilianza biashara hii ya damu," anasema.

Jasmin anasema damu huchukuliwa machinjioni na kuwekwa katika mapipa yenye ujazo wa lita 220, kisha huchemshwa na kukaushwa kwa siku tatu. Baada ya kukaushwa husagwa kwa kifaa maalumu.

"Damu hii huchemshwa kwa kutumia kuni na hutumia dakika 20 hadi 25 kubadilika kutoka hali ya kimiminika. Baada ya hapo hukaushwa kwa siku tatu hadi tano kutegemea na uwepo wa jua, kisha husagwa kwa kutumia kifaa maalumu na huwa tayari kwa ajili ya kwenda sokoni," anasema Jasmin.

Anasema kupitia uandaaji wa damu hiyo, watu takribani 150 wamejiajiri katika eneo la pembezoni mwa machinjio hayo.

Kupitia biashara hii imemwezesha kusomesha watoto wake wawili akiwa mlezi pekee wa familia baada ya mume wake kufariki dunia pamoja na kujenga nyumba mbili.

"Kupitia biashara hii ninasomesha watoto wawili katika shule binafsi, mmoja anasoma kidato cha tatu na mwingine yupo kidato cha kwanza. Pia nimeweza kujenga nyumba mbili huko Kilimanjaro," anasema.

Wakati naendelea kuzungumza mawili matatu na Jasmin, anajitokeza kijana aliyejitambulisha kama Nguzo Daudi (37) na kukazia juu ya namna ya uwepo wa machinjio hii ulivyowanufaisha.

"Tunaendesha maisha kupitia hii damu ambayo kwa hali ya kawaida unaweza kuona ni uchafu.

"Kila lita 220 ya damu ambayo tunanunua kwa Sh18,000 hadi 20,000 hutengeneza damu kilo 45 hadi 50 baada ya kuchakatwa. Kila kilo moja ya damu daraja la kwanza tunaiuza kwa Sh800 hadi 1,200 kwa kilo," anaeleza Nguzo na kuongeza:

"Daraja la pili ambayo huwa ni mabaki yaliyosalia baada ya kupatikana damu daraja la kwanza huuzwa kwa Sh400 hadi 500 kwa kilo."

Kupitia damu, Nguzo ambaye amedumu katika biashara hiyo tangu mwaka 2000, anasema imemwezesha kununua kiwanja eneo la Kivule chenye thamani ya Sh3.5 millioni pamoja na kuwasomesha watoto wake wawili pamoja na mdogo wake.

Nguzo anaeleza changamoto wanazokumbana nazo ni suala zima la mitaji pamoja eneo la kufanyia shughuli zao.

"Ukosefu wa mitaji ya kutosha unatukwamisha kufika mbali zaidi, pia tunashindwa kununua hata mashine za kisasa kwa ajili ya kufanyia shughuli zetu. Tunahitaji kuwezeshwa pamoja na mazingira tunayofanyia shughuli zetu si salama kwa afya zetu," anabainisha Nguzo.

Naye Andrea John (39) ameanza kujishughulisha na biashara ya kuuza makongoro tangu mwaka 2000 akiwa kijana mdogo ambaye hakufanikiwa kumaliza elimu ya kidato cha nne na kuishia kidato cha pili.

Kabla ya kuanza biashara ya makongoro, anasema alianza kuuza mifuko, biashara ambayo kwa kiasi fulani ilimsaidia kupata mtaji wa kuingia katika uuzaji wa makongoro.

"Nilipomaliza kidato cha pili nilishindwa kuendelea na shule kutokana na sababu za kiuchumi, niliona sielewi maisha nikaingia katika biashara ya kuuza mifuko enzi hizo, iliyonisaidia kupata mtaji wa biashara ya kongoro," anasema Andrea.

Kama ilivyokuwa kwa Jasmin, naye Andrea anasema aliirithi biashara hiyo kutoka kwa baba yake ambaye naye alikuwa akijihusisha na uuzaji wa makongoro.

"Biashara ya kuuza makongoro niliipenda mwenyewe, pia hata baba yangu alikuwa akijihusisha na biashara hii," anasema Andrea.

Nilipomuuliza sababu za kudumu katika biashara hiyo hadi sasa, Andrea anasema makongoro ni biashara inayoenda kwa haraka zaidi na pia ina faida.

Anasema wateja wake wakubwa ni wafanyabishara wanaouza chakula ambao huyatumia kwa ajili ya kutengeneza supu.

Andrea ambaye ni baba wa watoto wawili anaeleza kuwa biashara ya makongoro inamuwezesha kutimiza majukumu akiwa kama baba wa familia.

"Kupitia makongoro ninasomesha watoto wangu wawili; mmoja yuko kidato nne na mwingine yuko darasa la kwanza, pia nimefanikiwa kupata kiwanja ambacho kwa sasa nimeanza ujenzi," anasema Andrea.

"Kiufupi biashara hii ndio inayonifanya niendeshe maisha yangu hapa mjini," anasisitiza.

### Kipindi kigumu katika biashara

Andrea anasema tangu aanze biashara hiyo kipindi kigumu zaidi alichopitia ambacho kamwe hakitatoka kwenye akili yake ni kipindi ulipotokea ugonjwa wa rift valley.

"Yani siwezi sahau kile kipindi cha rift valley. Kilikuwa kipindi kigumu sana kwa sisi wafanyabiashara wa nyama na mazao yatokanao na hawa wanyama wanaochinjwa hapa. Nilikuwa sipati mteja wa kumuuzia hata kongoro moja kwa Sh200 Daaah...sitaki hata kukumbuka kwa kweli.

"Hata baada ya ugonjwa huo kutoweka watu bado walikuwa na hofu, hivyo tulikaa kwa muda mrefu bila shughuli ya kufanya," anaeleza.

Kwa mfanyabiashara yeyote lazima huwa kuna siku ambayo mauzo huwa makubwa kuliko siku nyingine. Kwa upande wa Andrea anasema siku za wikiendi ndio siku za neema kwake.

"Mwishoni mwa wiki ndio kipindi ambacho natengeneza faida nzuri kutokana na uwepo mkubwa wa bidhaa hiyo na kunifanya kununua kwa bei rahisi, pia wateja wengi," anaeleza.

Kuhusu changamoto, anaeleza kuwa kikwazo katika biashara yake ni ukosefu wa mahali salama pa kufanyia biashara pamoja na mtaji usiotosheleza kukuza biashara yake.

"Ningefurahi siku moja naamka najua naenda sehemu salama ya kufanyia biashara zangu. Hii ingenipa uhuru wa kufanya biashara zangu. Mazingira ya kuuzia si salama kutokana na kuwa kando kando ya barabara," anasema.

Andrea anawashauri vijana waliojifungia ndani wakilia ukosefu wa ajira, watoke nje na kutumia fursa zilizopo kujipatia riziki zitakazowawezesha kuendesha maisha yao.



Mchinjaji wa nyama ya mbuzi katika Machinjio ya Vingunguti akitayarisha nyama katika machinjio hayo. **Picha na Sunday George**



**MITAJI YA BIASHARA**

Andrea anasema wanaomba kuwezeshwa kwa kupewa mitaji yenye riba nafuu, ili waweze kukuza zaidi biashara zao.

"Hapa wengi tunafanya biashara kwa mitaji midogo ambayo inatukwamisha kufikia malengo makubwa ya biashara zetu, tunahitaji kuwezeshwa kwa kupata walau mikopo yenye riba nafuu na sisi tupo tayari kukaa vikundi," anasema Andrea.

**Sh800**

**Bei ya kilo moja ya damu daraja la kwanza.**



Mkazi wa Dar es Salaam akipakia damu ya ng'ombe iliyokaushwa katika machinjio Vingunguti jijini hapa. **Picha na Sunday George**